

Nafasi ya Tafsiri katika Ufundishaji wa Kiswahili: Mfano wa Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Upili nchini Uganda

Sarah Ndanu M. Ngesu
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ikisiri

Makala haya yanaangazia maoni ya walimu na wajifunzaji kuhusu matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda. Suala mojawapo linalozua mgogoro miongoni mwa wasomi, wataalamu, walimu na wajifunzaji wa lugha ni matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni na ya pili. Wanafunzi walioshiriki walikuwa wa kidato cha kwanza na cha pili. Data ilichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya umotishaji wa lugha iliyoasisiwa na Gardner (1985) na kuendelezwa na Dörnyei (1994). Matokeo yanaonesha kwamba tafsiri ina nafasi kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda. Aidha, imebainika kwamba tafsiri haiwezi kuepukika katika mazingira ya ufundishaji wa Kiswahili nchini Uganda. Hata, hivyo mbinu hii inapaswa kutumika pamoja na mbinu nyinginezo na kwa njia inayofaa.

Dhana Muhimu: tafsiri, ufundishaji, ujifunzaji, Kiswahili, Uganda

Utangulizi

Suala mojawapo linalozua mgogoro miongoni mwa wasomi, wataalamu, walimu na wajifunzaji wa lugha ni matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni na lugha ya pili. Kwa karne nyingi, tafsiri imepuuzwa kama mbinu muhimu ya ufundishaji wa lugha kutokana na kuhusishwa kwake na mbinu ya tafsiri-sarufi iliyotumika katika ufundishaji wa Kilatini na Kiyunani. Hata hivyo, matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha yanarejea kwa kasi katika karne hii ya 21. Watafiti na wataalamu (Duff, 1989; Cook, 2018) wanaoshadidia matumizi ya tafsiri kama njia muhimu ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni wanakubaliana kwamba ni zana inayowasaidia wajifunzaji kuelewa maneno na dhana za lugha lengwa. Wanaendelea kudai kwamba tafsiri ina nafasi kubwa katika elimu ya uwililugha na inajitegemea kama taaluma ya kiakademia. Makala haya yamejikita katika kuonesha mitazamo ya walimu na wajifunzaji kuhusu matumizi ya tafsiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Uganda.